

MIKOA YA TANZANIA BARA.

Na.	Mkoa
1	Arusha
2	Dar Es Salaam
3	Dodoma
4	Iringa
5	Kagera
6	Kigoma
7	Kilimanjaro
8	Lindi
9	Manyara
10	Mara
11	Mbeya
12	Morogoro
13	Mtwara
14	Mwanza
15	Pwani
16	Rukwa
17	Ruvuma
18	Shinyanga
19	Singida
20	Tabora
21	Tanga

MIKOA MIPYA ITAKAYOANZISHWA

- (i) **Mkoa wa Njombe** ambao unatokana na kumega na kuunganisha Wilaya za Njombe, Ludewa na Makete kutoka Mkoa wa Iringa. Mkoa huu utakuwa na Wilaya mpya ya Wanging'ombe ambayo inatokana na kugawanywa kwa Wilaya ya Njombe.
- (ii) **Mkoa wa Geita** ambao unatokana na kumega na kuunganisha Wilaya za Geita kutoka Mkoa wa Mwanza, Bukombe kutoka Mkoa wa Shinyanga na Chato kutoka Mkoa wa Kagera. Mkoa huu utakuwa na Wilaya mpya ya Nyang'hwale ambayo inatokana na kugawanywa kwa Wilaya ya Geita.
- (iii) **Mkoa wa Simiyu** ambao unatokana na kumega na kuunganisha Wilaya za Bariadi kutoka Mkoa wa Shinyanga, Maswa kutoka Mkoa wa Shinyanga, Meatu kutoka Mkoa wa Shinyanga na Wilaya mpya ya Busega kutoka Mkoa wa Mwanza. Mkoa huu utakuwa na Wilaya nyingine mpya ya Itilima ambayo inatokana na kugawanywa kwa Wilaya ya Bariadi.

- (iv) **Mkoa wa Katavi** ambao unatokana na kumega na kuunganisha Wilaya za Mpanda kutoka Mkoa wa Rukwa pamoja na Wilaya mpya ya Mlele ambayo inatokana na kugawanywa kwa Wilaya ya Mpanda.

MADHUMUNI YA KUANZISHWA MIKOA MIPYA

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaelekeza kuwa, kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za Serikali, Mheshimiwa Rais anaweza kuigawa Nchi katika Mikoa au Wilaya. Hivyo, madhumuni ya kuanzishwa kwa Mikoa hiyo ni kuboresha utendaji wa Serikali Kuu kwa kupunguza ukubwa wa maeneo ya Mikoa mama ili Wananchi wapate huduma za kiutawala ngazi ya Mikoa kwa karibu.

Jumla ya Mikoa ya Tanzania Bara itakuwa **25** ambayo ni Arusha, Dar Es Salaam, Dodoma, Iringa, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Mara, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Pwani, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga, Singida, Tabora, Tanga, Njombe, Geita, Simiyu na Katavi